## Maswali

1. Yosia alikuwa mfalme na umri gani?
2. Watu wengi waliabudu nini?
3. Yosia aliamua kufanya nini?
4. Yosia alifanya nini kwa Hekalu?
5. Nini ilipatikana kwa Hekalu?
6. Mbona Yosia aliogopa aliposikia maneno ya chuo?
7. Yosia aliita nani Yerusalemu? Alifanya nini?
8. Yosia alifanyaje sanamu na madhabahu?
9. Yosia alitimiza karamu gani Yerusalemu?
10. Yosia alikufa namna gani?

## Majibu

1. Yosia alikuwa mfalme na umri wa miaka 8.
2. Watu wengi waliabudu Baali na Ashtorethi, miungu wa uongo.
3. Yosia aliamua kusaidia watu wampende na kumtumikia Mungu.
4. Yosia alirekebisha na kusafisha Hekalu.
5. Chuo kizee cha Sheria za Mungu kilipatikana kwa Hekalu.
6. Chuo kilisema Mungu ataadhibu watu waovu.
7. Yosia aliita viongozi waje Yerusalemu. Chuo kilisomwa. Yosia aliahidi kutii Sheria za Mungu.
8. Yosia alifunja madhabahu na kuchoma hizo sanamu.
9. Yosia alitimiza karamu ya Pasaka huko Yerusalemu.
10. Yosia alienda kupigana na Wamisri. Alijeruhiwa. Alirudishwa Yerusalemu na akakufia kule.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 2 Mwaka wa 2

# 78 Yosia Mfalme Mzuri

### Kwa Biblia

2 Wafalme 22:1 – 13 na 2 Wafalme 23:1 – 4; 21 – 22; 29 – 30

### Kiini cha somo

Kuonyesha vile Yosia alijaribu kupenda na kumtii Mungu. Aliharibu uovu na akafundisha watu kuabudu Mungu kwa njia ya haki. Yosia alikuwa Mfalme mzuri aliyeamini Mungu

### Somo

Yosia alikuwa na umri wa miaka minane baba yake alipouawa. Yosia alikuwa mfalme alipokuwa na miaka minane. Yosia alikuwa amelelewa kumpenda Mungu. Yosia alitaka kuabudu na kumtii Mungu.

Wengi wa waliomshauri mfalme waliabudu Baali na Ashtorethi miungu za uongo. Ilikuwa vigumu mtoto wa miaka minane kupishana na watu wakubwa na wa nguvu. Watu wengi waliabudu hawa miungu wa uongo. Ilikuwa ngumu sana kwa kijana Yosia!

Yosia alikuwa mtoto sana. Lakini aliamua kwamba atamtumikia Mungu wakati wote. Aliamua kwamba atasaidia watu wake. Atawafundisha kumpenda Mungu. Yosia aliamini Mungu na Mungu alimsaidia. Ingawaje alikuwa mtoto lakini alikuwa na nguvu kwa sababu Mungu alimsaidia. Yosia alikuwa mmoja wa Wafalme wa Yuda waliokuwa na nguvu na kupendwa na Mungu.

Yosia alitaka kugomesha ibada ya sanamu. Alitaka kufundisha watu wamtumikie Mungu wa kweli.

Kwanza Yosia aliamru Hekalu kuu ya Mungu irekebishwe na isafishwe. Hekalu haikuwa ikitumiwa kwa sababu ya ibada ya sanamu. Ilikuwa chafu na imebomoka. Yosia alirekebisha Hekalu ili watu waweze kuabudu Mungu tena.

Kuhani Hilkia alipokuwa akitengeneza ndani ya chumba kimoja cha Hekalu, alipata chuo kizee sana. Aliita Shafani mwandishi. Shafani alimsomea hiyo chuo. Hiyo chuo ilikuwa nakala ya vitabu vya sheria vyenye Mungu alipea Musa. Labda kilikuwa kitabu cha Kumbukumbu ya Torati. Hilkia aliambia Shafani apelekee Mfalme na amsomee.



*Wakati huo waandishi walikuwa wakiandika kwa chuo. Chuo ni kipande kirefu cha ngozi na mwisho wa kila upande una mpini. Maandishi yalifanywa kwa sehemu, kipimo cha ukurasa wetu moja. Hiyo chuo ilifiringishwa ili kutafuta ukurasa mwingine. Sheria za Mungu ziliandikwa kwa chuo na kuwekwa vizuri. Wakati wa Wafalme waovu, watu waliabudu sanamu. Walisahau sheria za Mungu.*

Yosia alifurahi sana alipoona chuo iliyotoka Hekaluni. Alisikiliza kimakini wakati Shafani mwandishi alikuwa akimsomea chuo. Chuo kilisema adhabu yote yenye Mungu angeleta kwa watu wake kama watamuasi. Ilisema kwamba Mungu ataadhibu watu wakiabudu sanamu.

Yosia alifadhaika sana. Alijua watu walikuwa wameabudu sanamu kwa muda mrefu. Walikuwa wamekuwa waovu. Yosia aliuliza Hilkia kuhani aombe Mungu. Mungu alitumia Yosia ujumbe. Alisema, amekasirika sana kwa sababu watu walikuwa waovu sana. Lakini alijua kwamba Yosia alimpenda na alimtumikia. Mungu aliahidi kwamba hataadhibu watu wakati Yosia bado ni Mfalme.

Yosia alikusanya viongozi wote wa miji na vijiji. Aliwaleta Yerusalemu ili wasikilize maneno ya chuo. Chuo ilisomwa mbele ya kila mtu. Papo hapo kila mtu alisimama. Yosia alifanya ahadi. Yosia alijua lazima aangamize ibada ya sanamu. Alitaka kufundisha watu wake juu ya sheria za Mungu. Yosia alivunja madhabahu waliyotumiwa kuabudu sanamu Yerusalemu. Alichoma sanamu kwa Kijito cha Kidroni nje ya Yerusalemu. Alisafiri akizunguka nchi yote ya Yuda. Popote alienda alivunja hayo madhabahu na kuzichoma sanamu. Yosia alifunza watu kumpenda Mungu na kumtumikia.

Chuo kilizungumzia juu ya karamu ya Pasaka. Mungu aliamru watu wawe na karamu ya Pasaka kila mwaka. Kwa hiyo Pasaka watu walikumbuka vile Mungu aliwaokoa kutoka Misri utumwani. Walishukuru na kuabudu Mungu.

Yosia alijua watu walikua wamesahau kutimiza karamu ya Pasaka. Alikusanya watu wote Yerusalemu ili washerehekee karamu ya Pasaka. Yosia alifuata amri zote vile zilikuwa zimeandikwa kwa chuo. Yosia alipea watu wana kondoo wakule pamoja na mikate isiyotiwa chachu na mboga chungu vile Mungu alikuwa ameamrisha. Tangu wakati wa Samweli, hii ndiyo ilikuwa karamu ya Pasaka kubwa sana Yerusalemu.

Farao Neko, Mfalme wa Misri alienda na jeshi lake akipitia nchi ya Yuda. Farao alikuwa anaenda kupiga Mfalme wa Ashuru. Yosia alikuwa amehadhariswa kwamba asihuzeke na Wamisri. Lakini Yosia aliamua kujaribu kuzuia Wamisri. Yosia alienda na jeshi lake kupiga Wamisri. Yosia alipigana na Wamisri. Alijeruhiwa vibaya sana kwa hiyo vita. Yosia alibebwa kwa gari na kupelekwa Yerusalemu. Alikufia Yerusalemu.

Watu wote walia kwa kifo cha Yosia. Yosia alikuwa Mfalme mzuri sana. Aliamini Mungu. Aliharibu ibada ya sanamu. Alifundisha watu wake kumpenda Mungu na kumtumikia. Watu wote wa Yuda na Yerusalemu waliomboleza kwa ajili ya kifo cha Mfalme Yosia.